JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

# SHERIA BULLETIN

**Toleo la Kwanza**



# FANYENI KAZI KWA **UADILIFU**

## YALIYOJIRI


**01** **Fanyeni Kazi kwa Uadilifu:** Dkt. Ndumbaro

**02** **Makondo aongoza kikao Ghana**
Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo aongoza Kikao ....

**04** **Unaelewa nini kuhusu huduma ya msaada wa kisheria?**



## BODI YA UHARIRI

**MARY MAKONDO**
Katibu Mkuu

**LUSAJO MWAKABUKU**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAJUMBE**
George Mwakyembe | Farida Khalfani
William Mabusi | Felix Chakila

# FANYENI KAZI KWA UADILIFU:

## Dkt. Ndumbaro

**Na William Mabusi**

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro amewataka Watumishi wa umma kufanya kazi kwa uadilifu, weledi na ushirikiano katika maeneo yao ya kazi. Dkt. Ndumabaro ameyasema hayo wakati akitoa hotuba yake kufungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa RITA Jijini Arusha tarehe 21 Desemba, 2022.

Dkt. Ndumbaro amesema "tupige vita uzembe na rushwa sehemu zetu za kazi, na watumishi tuache ubadhilifu wa mali ya umma ili twende kwenye uzalishaji zaidi." Akiongelea falsafa ya uongozi wa Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuongeza uhuru wa wananchi kutoa maoni, Dkt Ndumbaro amesema "uhuru wa kutoa maoni unakaribisha ubunifu ambao huleta tija mahali pa kazi lakini nawaomba watumishi tutumie vema uhuru huo."

Katika hotuba yake Dkt. Ndumbaro ameagiza Mabaraza ya Wafanyakazi kudai haki na kujali uwajibikaji kwani haki inaenda na wajibu. Amewataka Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi kukemea uzembe, kusimamia nidhamu kazini na kuhakikisha kanuni na taratibu za utumishi wa umma zinafuatwa.

Akiongelea masuala mtambuka Dkt. Ndumaro amesema "magonjwa ya UVIKO-19 pamoja na UKIMWI bado yapo hivyo nawaomba watumishi tuendelee kuchukua kila aina ya tahadhari. Aidha, magonjwa ya kisukari na shinikizo la damu siyo ya kuambukiza lakini ni hatari sana." Magonjwa haya yanasababishwa kwa kiwango kikubwa na aina ya maisha tunayoishi ya kutozingatia ulaji mzuri, unywaji wa pombe kupindukia na kutofanya mazoezi, hivyo Dkt. Ndambaro amewaasa watumishi kujali afya zao kwa kula milo iliyokamilika, kunywa kwa kiasi na kufanya mazoezi.



*Dkt. Damas Ndumbaro Waziri wa Katiba na Sheria akihutubia kwenye Mkutanowa Baraza la Wafanyakazi wa RITA uliofanyika tarehe 17 Desemba, 2022 Jijini Arusha*




*Dkt. Damas Ndumbaro akishiriki katika wimbo wa "mshikamano daima" wakati wa mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa RITA, kulia kwake ni Mtendani Mkuu wa RITA Bi. Angela Anatory.*



Na Lusajo Mwakabuku - WKS

# MAKONDO AONGOZA KIKAO CHA WATAALAM WA HAKI NA SHERIA WA SERIKALI - GHANA




Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo aongoza Kikao cha dharula cha Saba cha Kamati ya Kitaalam ya Umoja wa Afrika cha Wataalam wa Sheria wa Serikali katika masuala ya haki na sheria kinachofanyika Accra nchini Ghana kilichoanza Tarehe 16 mpaka 19 Januari, 2023.

Mkutano huu una jukumu la kupitia, kuchambua na kuhakiki itifaki zitakazowasilishwa kwenye kikao cha Wakuu wa Nchi za Afrika Februari, 2023. Itifaki zinazoendelea kujadiliwa ni Itifaki ya Ushindani Afrika, Itifaki ya Haki za Miliki Ubunifu Afrika na Itifaki ya Uwekezaji Afrika.

Kamati hiyo ambayo ina ngazi ya Wataalam na ngazi ya Mawaziri, moja kati ya majukumu yake ni kuchambua na kupitisha Mikataba ya Kimataifa yote ambayo inawasilishwa kwa Wakuu wa Nchi kwa ajili ya kuridhiwa. Kwa upande wa Mawaziri, kamati hii inajumuisha Mawaziri wa Sheria na Wanasheria Wakuu, Mawaziri wenye dhamana ya Haki za Binadamu, Katiba na Utawala wa Sheria au Mawaziri au mamlaka nyingine zilizoidhinishwa ipasavyo na Serikali za Mataifa Wanachama.

Kamati ya wataalam inajumuisha Wataalam kutoka Nchi Wanachama wanaohusika na sekta zinazohusiana na masuala ya Haki na Sheria, ambayo mikutano yake hutangulia kabla ya mkutano wa ngazi ya Mawaziri.

Mwishoni mwa mwaka 2022, Tanzania ilichaguliwa katika Ukanda wa Afrika Mashariki kuwa Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Haki na Sheria ya Umoja wa Afrika kwa kipindi cha miaka miwili kutoka 2022 hadi 2024.

# Hatua Kali Zaidi Kuchukuliwa kwa Wahalifu wa Makosa ya Unyanyasaji Kijinsia:

Dkt. Ndumbaro




Dkt. Damas Ndumbaro Waziri wa Katiba na Sheria akihutubia kwenye maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia yaliyofanyika katika viwanja vya Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (TLS) Desemba 5, 2022 Jijini Dar es Salaam.

**Na William Mabusi - WKS**

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro amesema Serikali imejipanga kuchukua hatua kali zaidi kwa wahalifu wa makosa ya unyanyasaji kijinsia. Waziri Ndumbaro ameyasema hayo wakati akihutubia kwenye maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia yaliyofanyika katika viwanja vya Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (TLS) Desemba 5, 2022 Jijini Dar es Salaam.

Dkt. Ndumaro amesema "rai ya Serikali ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuendelea kupaza sauti siku zote 365 za mwaka kutambua viashiria vya unyanyasaji wa kijinsia na kuvitolea taarifa kwenye vyombo husika ili sheria ichukue mkondo wake."

Katika hatua nyingine Mhe. Ndumbaro amesema "Wizara ya Katiba na Sheria iko mbioni kuanzisha usajili wa mtandaoni (online registry) kwa mtu ambaye amethibitishwa na Mahakama kuwa na hatia ya unyanyasaji wa kijinsia." Watu watakaokuwa katika orodha hiyo hawatakuwa na uwezo wa kukopa benki wala kupata ajira, miongoni mwa huduma zingine.

Naye Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo akitoa salaam katika maadhimisho hayo amesema hatua zitaendelea kuchukuliwa kwa wahusika wa matukio ya ukatili wa kijinsia yanayoripotiwa. Bi Makondo amesema "Juhudi za Serikali ni kutokomeza ukatili wa kijinsia hivyo wananchi tuiunge mkono Serikali kwa kutoa taarifa za matukio hayo."

Vile vile Bi. Kathrin Steinbrenner Naibu Balozi wa Ujerumani nchini amesema harakati za kupigania haki ni kwa makundi yote wanawake, watoto na wanaume kwani makundi yote yanapitia ukatili wa kijinsia. Amempongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mstari wa mbele na kuwa mfano wa kuigwa katika kutetea haki za binadamu ambapo Ujerumani inaungana na Tanzania katika vita ya kupinga ukatili wa kijinsia.

Akitoa salaam za ukaribisho, Jaji Dkt. Benhaji Masoud Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo amesema ukatili na unyanyasaji wa kijinsia si tu una athari kwa wahusika bali pia unaathiri maendeleo ya Taifa. Amesema Taasisi yake iko tayari kupambana na vita vya ukatili wa kijinsia ili kuwa na jamii salama na yenye maendeleo.




*Sehemu ya washiriki kwenye maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia*


Mawakili kutoka Chama cha Wanasheria (Tanganyika Law Society) wakiwa wanatoa huduma ya msaada wa kisheria katika kata ya Ngarenanyuki Wilaya ya Meru.

# UNAELEWA NINI KUHUSU HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA?

Na. George Mwakyembe & Lusajo Mwakabuku - WKS

## Huduma ya Msaada wa Kisheria ni nini?

Huduma ya Msaada wa Kisheria ni huduma inayotelewa kwa wananchi ambao hawamudu gharama za kuwalipa mawakili kwa ajili ya kuendesha kesi, lakini si hivyo tu bali ni mkakati ambao unaratibiwa na Wizara ya Katiba na Sheria kwa ajili ya kuwapa elimu wananchi juu ya masuala ya sheria mbali mbali kama vile sheria za mirathi, sheria za ndoa, sheria zinazohusu ardhi pamoja na sheria zingine ili kuweza kuzifahamu na kuzitumia katika maisha yao ya kila siku. Huduma ya msaada wakisheria imekuwa mkombozi kwa wananchi wengi ambao wana kipato cha chini.

## Kuna masharti gani katika kupata huduma hii?

Sheria hii imeweka masharti ya utaratibu wa kutoa msaada wa kisheria kwa watu wanaosaidiwa. Hivyo anayehitaji kusaidiwa anapaswa kufanya maombi kwa mtoa huduma ya msaada wa kisheria. Hivyo basi taasisi ya utoaji wa huduma za kisheria itaangalia sifa za mwombaji kulingana na taratibu za taasisi husika. Maombi ya msaada wa kisheria yatafanywa na Mhitaji mwenyewe au mwakilishi wake aliyemteua au shirika kwa niaba ya mtu anayehitaji kusaidiwa ambaye hana uwezo wa kulipa gharama za mawakili wa kujitegemea.

Kwa masharti ya sheria hii msaada wa Kisheria utatolewa na taasisi tu ambayo imesajiliwa na sio watu binafsi. Hivyo basi mawakili, wanasheria na wasaidizi wa kisheria watatoa huduma ya msaada wa kisheria kwa niaba ya taasisi husika. Mtu yeyote atakayekiuka utaratibu uliowekwa nasheria kuhusiana na utoaji wa msaada kisheria kupitia taasisi atakuwa ametenda kosa na adhabu yake itakuwa faini ya shilingi milioni tano au kifungo cha mwaka mmoja jela au vyote viwili.

Pia mtu yeyote atakayetoza fedha kinyume na sheria atakuwa ametenda kosa na adhabu yake itakuwa faini isiyopungua shilingi milioni mbili au kifungo kisichopungua miezi sita jela au vyote viwili. Pamoja na adhabu iliyotajwa hapo juu, mtu huyo atatakiwa pia kurejesha fedha alizochukua kwa mteja wake.


Bi, Ekael Pallangyo kutoka chama cha wanasheria (Tanzania Women Lawyer Association) akiwa anatoa maelezo kwa Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Eng, Richard Ruyango alipetembelea kwenye banda wakatika wa kutoa huduma ya msaada wa kisheria katika kata ya Ngarenanyuki.

## Nini ni chanzo cha Sheria hii?

Chimbuko la sheria hii lilitokana na uhitaji mkubwa wa kuwa na sheria nchini itakayoongoza kisheria namna ya utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa wahitaji ili waweze kufikia haki. Sheria hii ilitungwa na bunge mnamo tarehe 31 Januari, 2017, ikapitishwa rasmi na kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 21 Februari, 2017. Ilitanganzwa kwenye gazeti Serikali namba 9 la 2017 na kuanza kutumika rasmi Tarehe 1 Julai, 2017 kwa mujibu wa tangazo la serikali namba 20 la mwaka 2017. Pia sheria hii imetungwa kukidhi matakwa ya mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo nchi yetu imesaini na kuridhia kuhusu haki za binadamu ikiwemo haki ya kupata msaada wa kisheria.

Sheria inampa mamlaka Waziri wa Katiba na Sheria kutengeneza kanuni za utekelezaji wa sheria hii. Pia sheria hii inafuta sheria ya msaada wa sheria (Mwenendo wa Makosa ya jinai) Sura ya 21. Bila kuathiri masharti ya sheria hii amri zote, kanuni, miongozo, na maagizo yaliyofanywa chini ya sheria iliyofutwa yataendelea kuwa na nguvu ya kisheria hadi pale kanuni mpya zitakapotengenezwa na kuanza kutumika rasmi.

## Nani anaweza kusajiliwa kutoa huduma hii?

Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria ndio ana mamlaka ya kuteua Wasajili wasaidizi miongoni mwa watumishi wa umma ili kurahisisha usajili wa watoa huduma za msaada wa kisheria katika ngazi za mkoa na wilaya ambao watawajibika kwa Msajili. Watakuwa wana jukumu la kusajili watoa huduma za msaada wa kisheria na kutoa vyeti vya usajili kwa niaba ya Msajili isipokuwa hawatakuwa na mamlaka ya usajili wa taasisi inayoomba kutoa huduma zaidi ya mkoa au wilaya husika. Wizara inahimiza kujisajili kwa taasisi zote nchini zinazotoa huduma ya msaada wa kisheria ambalo ni jukumu la msingi la Wizara ya Katiba na Sheria kwa mujibu wa sheria ya mwaka 2017.

Aidha, Wizara imeweka mfumo wa kielektroniki ambao ni *www.legaid.sheria.go.tz* mfumo huu unapokea maombi ya kujisajili watoa huduma wa msaada wa kisheria, na mfumo huu pia unatambua maeneo yao na kuwarahisishia wale wanaotaka huduma za msaada wa kisheria .

# Serikali Yaahidi Kuboresha Upatikanaji Wa Haki Za Binadamu.

**Na William Mabusi & Lusajo Mwakabuku - WKS**



*Jaji Imani Daud Aboud ambaye pia ni Jaji wa Mahakama Kuu nchini Tanzania aliteuliwa Mei 2021 kuwa Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na amekuwa mwanamke wa pili kushika wadhifa huo mkubwa katika Mahakama hiyo.*



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro akizungumza na Jaji Imani Daud Aboud ambaye pia ni Jaji wa Mahakama Kuu nchini Tanzania walipokutana mwanzoni mwa mwezi Januari*

Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria imeihakikishia Mahakama ya Afrika inayoshughulika na haki za binadamu kuwa inathamini mchango mkubwa unaotolewa na Mahakama hiyo katika kulinda na kutetea haki za binadamu na kwamba ipo tayari kushirikiana Mahakama hiyo katika kushughulikia masuala yote yahusuyo haki za binadamu.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb) Tarehe 11, Januari 2022 Jijini Dar es Salaam alipokutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu Mhe. Jaji Iman Daudi Aboud huku akibainisha mipango ya Serikali katika kuchangia upatikanaji wa haki za binadamu.

Aidha katika mazungumzo yao, Waziri Ndumbaro ameeleza kuwa Serikali inachukulia kwa uzito mkubwa uwepo wa Mahakama hiyo nchini ikizingatiwa kuwa Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imeyapa umuhimu na uzito mkubwa masuala yote yahusuyo haki za Binadamu.

Kwa upande wake Jaji Aboud, yeye alizungumzia zaidi masuala mbalimbali yahusuyo Haki za Binadamu nchini na namna bora ya kuendeleza ushirikiano kati ya Serikali na Mahakama. Mhe. Ndumbaro akamweleza kuwa Wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaendelea kufanya mchakato wa ujenzi wa jengo la kudumu la Mahakama hiyo na kwamba amepanga kuitembelea Mahakama hiyo hivi karibuni.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Haki za Binadamu Bw. Richard Kilanga kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Bw. Hangi Chang'a Mkurugenzi Msaidizi sehemu ya Katiba, Haki za Binadamu na Mashauri ya Uchaguzi na Bi. Vivian Method Wakili wa Serikali Mwandamizi wote kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Mtanzania Jaji Imani Daud Aboud ambaye pia ni Jaji wa Mahakama Kuu nchini Tanzania aliteuliwa Mei 2021 kuwa Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu Watu yenye Makao yake Makuu jijini Arusha. Jaji Imani amekuwa mwanamke wa pili kushika wadhifa huo mkubwa katika Mahakama hiyo.

# Matukio katika Picha




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo akishiriki katika kikao cha Kamati Maalum ya Haki na Sheria ya Umoja wa Afrika, Jijini Addis Ababa.*




*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro katika kikao cha Nane cha Kamati ya Watalaam ngazi ya Mawaziri wa Masuala ya Haki na Sheria kutoka nchi wanachama wa Umoja wa Afrika akipongezwa mara baada ya Tanzania kuchaguliwa kuwa mwenyekiti wa kikao hicho kuanzia 2022 mpaka 2024. Kikao hicho kilichofanyika Jijini Addis Ababa, Ethiopia.*



*Dkt. Damas Ndumbaro Waziri wa Katiba na Sheria katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa RITA*



*Wananchi wa Kata ya Ngarenanyuki katika Halmashauri ya Meru wakiwa wamejitokeza kupata Huduma ya Msaada wa Kisheria  viwanja vya Ngarenanyuki.*




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria akiendesha kikao cha saba cha Kamati ya Kitaalam ya Umoja wa Afrika cha Wataalam wa Sheria wa Serikali katika masuala ya haki na sheria.*



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro na Jaji Imani Daud Aboud katika picha ya pamoja na wajumbe walioshiriki kikao.*




*Bi. Mary Makondo Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria (wa tatu kushoto) wengine kutoka kushoto ni Katharina Kuehn Mratibu wa Mradi wa Upatikanji haki kwa Wanawake na Wasichana unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Bi. Felistas Mushi Kaimu Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma ya msaada wa Kisheria na kulia kabisa ni Bi. Maria Kwambaza Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Sera na Mipango Wizara ya Katiba na Sheria.*